TANGAZO LA SERIKALI Na. 243 la tarehe 4/4/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA USHURU WA MAZAO YA UVUVI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KALAMBO YA MWAKA 2025

Jina

TS Na. 815 la 2024

**1.** Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ushuru wa Mazao ya Uvuvi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ushuru wa Mazao ya Uvuvi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ya mwaka 2024 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 3

**2.** Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika kanuni ya 3 kwenye tafsiri ya maneno "Afisa Mwidhiniwa" kwa kuongeza maneno "na Mkurugenzi" baada ya maneno "aliyeteuliwa".

Marekebisho ya kanuni ya 5

**3.** Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika kanuni ya 5 kwa-

(a) kufuta na kuandika upya maelezo ya pembeni kama ifuatavyo:

"Kibali cha kufanya shughuli za uvuvi";

(b) kufuta maneno "kukasanya ushuru wa mazao ya uvuvi" yaliyo katika kanuni ndogo ya (1) na badala yake kuweka maneno "kufanya shughuli za uvuvi".

Marekebisho ya kanuni ya 9

**4.** Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika kanuni ya 9, kwa-

(a) kufuta na kuandika upya kanuni ndogo ya (3) kama ifuatavyo:

"(3) Endapo mmiliki wa chombo atashindwa kulipia chombo chake ndani ya siku thelathini baada ya kukamatwa kwa chombo hicho, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kukitaifisha na kukiuza baada ya kupata idhini ya mahakama, na fedha itakayopatikana italipia ada ya usajili, faini pamoja na gharama za kukamata na kiasi kinachobaki kitarudishwa kwa mmiliki"; na

(b) kuongeza kanuni ndogo zifuatazo mara baada ya kanuni ndogo ya (3):

"(4) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (3), kabla ya kuuza chombo kilichokamatwa, Mkurugenzi atatoa notisi ya siku saba kwa mdaiwa na umma kuhusiana na kusudio la kuuza chombo hicho.

(5) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote itakayotokea wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa kwa uzembe wa watumishi wa Halmashauri au Wakala.".

Marekebisho ya kanuni ya 10

**5.** Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika kanuni ya 10 kwa kufuta na kuandika upya kanuni ndogo ya (2) kama ifuatavyo:

"(2) Chombo ambacho kitafanya shughuli za uvuvi wakati namba ya usajili imejirudia kitahesabika kuwa hakijasajiliwa na utaratibu wa adhabu utakaotumika kwa mmiliki wa chombo hicho utakuwa ule ulioainishwa katika kanuni ya 9 ya Sheria Ndogo hii.".

Marekebisho ya kanuni ya 12

**6.** Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika kanuni ya 12 kwa kuongeza maneno "atakuwa ametenda kosa endapo" baada ya maneno "mtu yeyote".

Marekebisho ya Jedwali la

**7.** Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika Jedwali

Pili

la Pili kwa kufuta maneno “Kibali cha kukusanya ushuru” na badala yake kuweka maneno “Kibali cha kufanya shughuli za uvuvi”.

“Makosa

**12**. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo-

(a) atatoka nje ya eneo la Halmashauri na kufanya shughuli za uvuvi bila kutoa taarifa kwa Kitengo cha Usimamizi wa Mialo na kupata kibali;

(b) atafanya shughuli za ukusanyaji, utengenezaji na usafirishaji wa samaki wabichi, wa kubanikwa kwa moshi, jua au chumvi bila ya kuwa na kibali cha Halmashauri;

(c) atapakia au kusafirisha mzigo wowote wa samaki, mabondo au bidhaa nyinginezo zitokanazo na mazao ya uvuvi kutoka mwaloni au eneo lolote la Halmashauri bila ya kulipiwa ushuru wa mazao ya uvuvi;

(d) atavua samaki kwa kutumia nyavu zisizoruhusiwa;

(e) atavua au kuua samaki wadogo ambao hawajakua kufikia kiwango cha kuvuliwa.

(f) atafanya shughuli za uvuvi na kusafirisha samaki nyakati za usiku bila ya kulipia ushuru;

(g) atamzuia, kumgomea au kumshambulia Afisa uvuvi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala wakati anapotekeleza mojawapo ya majukumu yao;

(h) atafanya biashara ya uvuvi au kuuza samaki au mazao yatokanayo na samaki bila leseni;

(i) atasafirisha samaki wabichi ambao watathibitika wana madhara kwa mlaji.

(j) atalima mazao ya chakula ndani ya ziwa na matumizi ya dawa zenye sumu za magugu na wadudu;

(k) atauuza samaki wabichi na wakavu katika maeneo yasiyoruhusiwa kama barabarani bila kujali afya ya mlaji.”.

Marekebisho ya Jedwali la Tatu

**8.** Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika Jedwali la Tatu kwa kufuta maneno “au matumizi ya nyumbani”.

Dodoma
12 Machi, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi- OR-TAMISEMI*